# UTENZI WA UKOMBOZI WA ZANZIBAR

*Euphrase Kezilahabi*

*Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* ni kitabu kilichotungwa na Muhammed S. Khatib na kuchapishwa na Oxford University Press mnamo 1975. Katika Utangulizi ulioandikwa na Shekh Thabit Kombo - aliyekuwa katibu Mkuu wa Chama cha Afro - Shirazi, tunasoma maneno haya:-

> Hiki ni kitabu kinachofaa sana kusomwa si na watoto au vijana wetu tu, bali hata watu wazima, ili kujua ukweli wa mambo. Kwa hiyo wataweza kulinganisha hali ya maisha mabaya ya kutawaliwa na faraja ya kujitawala.

Ni kweli kabisa kuwa *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* unahusu ukweli wa historia ya Zanzibar, ukweli wa kisiasa na hasa ukweli kuhusu Chama cha Afro-Shirazi, jinsi kilivyodhulumiwa na wakoloni wakati wa harakati za ukombozi na jinsi kilivyowaendeleza watu baada ya mapinduzi. Baada ya kusoma utenzi huu msomaji anaweza kuona dhahiri kuwa mapinduzi ya mwaka 1964 yalikuwa halali na ya lazima baada ya njia za utaratibu wa kisiasa - yaani kura - kushindikana. Katika kuujadili utenzi huu tutaugawa katika sehemu nne zifuatazo:

(a) wakati kabla ya kufika kwa wageni,
(b) wakati wa utawala wa kigeni,
(c) wakati wa harakati za ukombozi,
(d) wakati baada ya mapinduzi

Mwishoni mwa mjadala wetu tutauchambua utenzi kisanaa ili kuona uwezo na udhaifu wa mwandishi katika kutumia sanaa hii ya utenzi kutoa mawazo yake.

### (a) Wakati kabla ya kufika kwa wageni.

Sehemu hii inaanzia ubeti wa 31 mwandishi anapoeleza jinsi visiwa vya Unguja na Pemba vilivyokuwa vimeungana na bara.

Kisiwa hiki Unguja
Na Pemba unayotaja
Viliungana pamoja
Ardhi moja sawiya.

Huu ni ubeti muhimu. Linganisha ubeti huu na ubeti wa 491 usemao:

Nyerere pamwe Karume
Viongozi wanaume
Waliungana kwa shime
Nchi yetu kuwa moya.

Itaonekana wazi kuwa hapo zamani visiwa hivi viwili viliungana na bara; kwa hiyo muungano wake wa kisiasa uliofuata baadaye ulikuwa na mizizi katika historia na jiografia ya nchi hizi mbili - Zanzibar na Tanganyika. Mwandishi ametumia muda wa kutosha kueleza jambo hili.

Katika sehemu hii ya kwanza mwandishi ametumia mtindo wa fasihi simulizi. Kwa kutumia mtindo huu amevuka mpaka wa hali halisi na kuingia katika ulimwengu wa kubuni. Ndio maana hatupewi tarehe mahususi za kihistoria au maelezo thabiti. Kwa hiyo mwandishi hategemei msomaji aulize "ni lini nchi hizi zilitengana?" Jibu lake ni "zamani sana." Mwandishi anafikiria hata jinsi ndege walivyokuwa wanarukaruka:

Ndege wote warukao
Kwa maringo na matao
Mote humu ndimo mwao
Watuka bila udhia.

Waweza lala Ujiji
Wakamkia Rufiji
Tena wakahama mji
Pemba wakachomozeya.

Beti hizi ndizo zinazoupa utenzi huu uhai kisanaa na zinamsukuma mbele msomaji. Mwandishi anaendelea kutueleza jinsi wavuvi walivyohamia visiwani. Hadithi ya kurudi mrima kuoa imeelezwa vizuri. Masimulizi ya kifasihi-simulizi yanapungua kadiri mwandishi anavyoendelea. Tunapofika ubeti wa 86 tunaanza kupata ushahidi thabiti; majina ya watu yanaanza kutajwa na tarehe zinatolewa.

Katika ubeti huo tunaelezwa kuwa kiongozi wa kwanza alitokeza mwaka wa 1975. Baada ya hapo tarehe za watawala mbalimbali zinatajwa. Mlolongo huu wa watawala unakwisha Seyyid Saidi anapohamia Zanzibar. Hapa tunafikia mwisho wa sehemu hii ya kwanza.

Katika sehemu hii mwandishi ameonyesha kuwa kabla ya kufika kwa wageni wananchi wa visiwa hivi waliishi vizuri bila ya migogoro mikubwa. Mgogoro pekee uliotokea ni ule wa Pemba kutaka utawala wao wenyewe mnamo 1400 (ubeti wa 90).

(b) **Wakati wa utawala wa kigeni.**

Kufuatana na maelezo ya mwandishi utawala wa kigeni unaanza kuota mizizi mwaka wa 1832 wakati Seyyid Saidi anapohamia Zanzibar. Sababu zilizomfanya ahamie Zanzibar ni kama zifuatazo: amani - (iliyokuwako Unguja), maji matamu, habari shwari, rutuba ya nchi na biashara. Sababu hizi zimetajwa katika beti za 122—126. Lakini sababu muhimu tunaziona zikitajwa katika beti za 129 na 130.

Utumwa ukazaliwa
Watu wakanunuliwa
Na hata kuadhibiwa
Shida kuwalemeya.

Wenyeji wakafurushwa
Mashambani kulimishwa
Kwa mateso wakachoshwa
Wengine wakajifiya.

Kwa hiyo kuja kwa Waarabu kulifuatiwa na mateso na unyonyaji wa kiuchumi. Beti nyingi zinazofuata zinaeleza uonevu ulifanywa na masultani mbalimbali hasa Bargash na Khalifa. Tunaelezwa kuwa Khalifa ndiye aliyewakaribisha Wahindi nchini, wakaanza kuwanyonya watu kwa kufungua maduka na kuuza kanzu. Jitihada za Mwingereza kuzuia biashara ya utumwa zinagusiwa. Uonevu wa Mwafrika unafikia upeo wake katika beti za 256—281.

Tunaelezwa hali ya ubaguzi iliyokuwepo ubaguzi wa elimu na ubaguzi wa matibabu. Kuhusu ubaguzi wa elimu mwandishi anasema:

Na waliobahatika
Chumba cha nane kufika
Walifika kwa mashaka
Tena wachache sikiya.

Na kuhusu matibabu anatwambia:

Wanyonge wakifiana
Kila siku wengi sana
Kukosa tiba ya maana
Itayowasaidiya.

Mambo haya yanagusiwa tena katika beti za 266 - 268. Unyonyaji wa kiuchumi unajadiliwa tena katika beti za 277 - 280. Beti hizi zinaonyesha jinsi njia zote za uchumi zilivyokuwa mikononi mwa mabepari. Viwanda, benki na mashirika mbalimbali ya uchumi vilishikwa na wadhalimu hawa. Kwa jumla sehemu hii ya pili ndiyo inayosikitisha zaidi kuliko sehemu zingine.

**(c) Wakati wa harakati za ukombozi.**

Sehemu hii ndiyo inayotupa ukweli kuhusu ulaghai wa Mwingereza na hila zake. Sehemu hii inaanzia ubeti wa 299.

Baadaye Waafrika
Ghafula wakaamka
Ikawa wajumuika
Kila kitu kwa pamoya.

Katika sehemu hii mwandishi amejitahidi kuonyesha kuwa Chama cha Afro-Shirazi toka siku zake za mwanzo kilikuwa Chama cha walio wengi Zanzibar. Sehemu hii inaonyesha juhudi za Mwingereza katika kuzuia wimbi la harakati za Uhuru. Mwandishi ameieleza historia ya Afro-Shirazi kwa ufupi. Historia hii inasisimua hasa kwa mtu ambaye ndiyo kwanza anasikia habari hizi. Katika ubeti wa 303 mwandishi anatueleza kuwa umoja wa Waafrika ulianzia katika klabu ya mpira. Klabu hii iliunda umoja ulioitwa 'African Association' mnamo 1935. Mwanzoni serikali ya Mwingereza ilikataa kuutambua umoja huu; ikakataa kutoa kibali cha kujiandikisha. Baadaye iliruhusu kuandikishwa kwa umoja huo lakini ikafanya njama za kukizuia Chama kisiendelee. Kwa njama hizi tunaona Chama kinagawanyika, pakatokea Afro na Shirazi - vyama viwili (ubeti 322). Mnamo tarehe 5 Februari, 1957 vyama hivi viliungana tena na kuwa Chama kimoja kilichoitwa 'Afro-Shirazi Party.' Nao walowezi Sultani na Wahindi kwa msaada wa Waingereza walianzisha Chama chao kilichoitwa 'Hizbu.'

| | |
|---|---|
| Sultani na Hizbu | Waliipa kila zana |
| Walikuwa masahibu | Kila wanapokutana |
| Mwingereza mahabubu | Ili waweze shindana |
| Na yeye akajitiya | Na Afro-Shiraziya |

Katika beti zinazofuata tunaona Chama cha Afro-Shirazi kikigawanyika tena - Afro-Shirazi na 'Zanzibar and Pemba Peoples Party' (Z.P.P.P.). Hiki cha pili kiliongozwa na Shamte. Kukawa na Vyama vitatu Zanzibar - Vyama ambavyo vilianza kupambanishwa ili kuchagua Chama ambacho kingetawala. Katika uchaguzi Afro-Shirazi ilikuwa na alama ya Kisima, Hizbu Jogoo, na Z.P.P.P. samaki. Katika uchaguzi wa kwanza tunaona Afro-Shirazi inashinda lakini inadhulumiwa. Badala ya kupewa nafasi ya kuunda serikali, Mwingereza anaamuru iundwe serikali ya mseto wa vyama vyote vitatu. Kura zilipigwa tena na matokeo yakawa: Afro viti 10, Hizbu viti 10 na Z.P.P.P. viti 3. Katika beti zinazofuata Afro inashitakiwa kuwa ilifanya ghasia wakati wa uchaguzi. Chini ya utetezi wa wakili Swanzy kutoka Ghana, Afro inashinda kesi.

Mwaka 1963 uchaguzi unaitishwa tena. Hizbu na Z.P.P.P. zinafanya mbinu za kuungana ili kuishinda Afro. Muungano huu unawapa viti 18 na Afro 13. Mwingereza anaomba Chama kilichoshinda kiunde serikali. Upesi upesi wanapewa uhuru tarehe 9 Desemba, 1963 chini ya bendera ya Sultani. Kama mwandishi anavyoeleza hii haikuwa serikali ya watu. Ilikuwa serikali karagosi iliyokuwa bado chini ya uongozi wa Mwingereza.

Mwingereza kawa Bwana
Wa kumpinga hapana
Akatutawala tena
Lolote kujifanyia.

Mpaka hapa tunaona kuwa harakati za kujikomboa zilikuwa zikifuata utaratibu uliokuwa umewekwa. Wananchi waling'amua kuwa utaratibu wa kura haungeweza kuwafikisha mbali. Usiku wa kuamkia tarehe 12 Januari, 1964 wananchi, chini ya uongozi wa Abeid Karume wanafanya *mapinduzi*. Walikata shauri kutumia silaha kujikomboa baada ya mbinu za kidemokrasi kushindikana. Hapa tunafika mwisho wa sehemu ya tatu.

### (d) **Wakati baada ya Mapinduzi.**

Sehemu hii ndiyo ya maana sana katika utenzi. Mwandishi ameipa nafasi kubwa ya kutosha. Sehemu hii ingeweza kuitwa 'sifa za Karume.' Katika sehemu hii mwandishi ameorodhesha mambo mazuri ambayo yamefanywa na marehemu Abeid Karume katika kuiendeleza Zanzibar. Baadhi ya mambo hayo ni: kuondoshwa kwa rehani (460); kutumika kwa lugha ya Kiswahili maofisini (466); kuwepo kwa Chama kimoja tu cha siasa nchini yaani *Afro-Shirazi* (475); kutaifishwa kwa ardhi (478); wazee walijengewa nyumba (481); kutunzwa kwa wasiojiweza na watoto yatima (610—611); kuondoshwa kwa Kombora la Marekani (485); Muungano wa Zanzibar na Tanganyika (490—495); kutaifishwa kwa shule zote na kutoa elimu bure (497—499); kuondoshwa kwa ubaguzi wa kabila na rangi (527—528, 749—752); kuzuiwa kwa watoto kufanya biashara ndogo ndogo za mitaani na kazi za uboi (536); kuchomwa moto rikishoo zote (540—544); kufunguliwa kwa maduka ya serikali ili kuondosha unyonyaji, kwa kitendo hiki maduka ya mabepari yaliangamia na serikali ikashika biashara zote za ndani na nje (552—260); kujengwa kwa viwanda k.m. kiwanda cha viatu (565) sigara (567); matrekta (606) maziwa (608), na vile vile viwanda vidogo vidogo vya matunda, samaki, biskuti, mafuta, sabuni n.k.; kujengwa kwa miji mipya k.m. Kikwajuni,

Kilimani, Michenzani, Wete, Chakechake Mkoani, Micheweni, Makunduchi, zaidi ya hayo ujenzi wa Bwawani, gati la meli, viwanja vya ndege na mtambo wa televisheni; kukomeshwa kabisa kwa unyang'anyi; wizi, ulevi na uvutaji bangi (643—655), ukahaba (662) na hongo (671).

Haya ni baadhi tu ya mambo muhimu yaliyofanywa na Abeid Karume. Sehemu hii inakwisha kwa masikitiko - kifo cha Karume - (709—727):

Ilikuwa ni jioni
Kumi na mbili za zoni
Lipofika mahaini
Kwa kitendo cha ubaya.

Walingia ukumbini
Uliopo hapo chini
Na silaha mikononi
Ghafula wakavamiya

Katika ubeti wa 720 tunaelezwa kifo chake.

Karume walimuuwa
Roho yake liitowa
Muda haikuchukuwa
Mauti yakamjiya.

Hapa tunafika mwisho wa sehemu ya nne. Beti zinazofuata ni maombolezo na dua kwa Rais Jumbe.

### (c) Hatima

Kisanaa utenzi huu unafuata kanuni za uandishi wa tenzi. Ni utenzi wa kawaida wenye mistari minne na bahari ya -ya-. Bahari hii imetumika katika tenzi nyingi sana. Mizani ni nane kama kawaida. Muundo wa utenzi ni ule ule wa mapokeo wa kuanza na *sala* (1 - 16) halafu unafuata *utangulizi* (17—20) unaofuatiwa na *habari kamili*. Mwishoni mwa utenzi kuna *dua, maombi* ya mwandishi ya kusahihishwa kama amefanya kosa. Tofauti ni kwamba mwandishi hataji *jina* lake mwishoni mwa utenzi lakini mwisho ndio ule ule wa:

Kalamu hapa naweka
Na maneno kufungika
Patosha nilipofika
Kwa herini nawambiya.

Kufuatana na kanuni za utenzi ni utenzi mzuri ambao hauna dosari za upungufu wa mizani au kuzidisha. Lakini inaonekana dhahiri kuwa ni mwandishi ambaye hajakomaa sana katika ushairi. Wakati mwingine mwandishi anaandika beti dhaifu kwa mfano ubeti wa 427:

Uhuru wa mabwanyenye
Wanaoishi kwa unyenye
Ndio watu hasa wenye
Mali na mashamba piya.

Mstari wa tatu si wa kawaida katika uandishi wa tenzi. Maana ya mstari huo haikutosheleza sawa sawa; inategemea sana msitari unaofuata. Labda kisanaa udhaifu mkubwa wa mwandishi ni kuwa ametumia mtindo wa maelezo toka mwanzo hadi mwisho. Hatumii mbinu za mazungumzo kama vile alivyotumia kwa

mfano mwandishi wa *Utenzi wa Adamu na Hawa* mbinu ambazo zinafanya utenzi uwe hai. Wahusika tuwaonao katika utenzi huu hawana uhai, tunaelezwa tu matendo yao.

*Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* ni utenzi wa kihistoria. Mifano michache ya tenzi kama hizo ni kama ifuatayo: *Utenzi wa vita vya Uhud, Utenzi wa Vita vya Wadachi kutamalaki Mrima, Utenzi wa Vita vya Uhuru; Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika, Utenzi wa Jamhuri ya Tanzania, Utenzi wa Zinduko la Ujamaa, n.k.*

Tenzi za kihistoria mara nyingi hutegemea sana ukweli uliotokea. Tenzi za aina hii hupungua uzito zinapopotosha ukweli (labda mwandishi mwenyewe aeleze kuwa anafanya hivyo kwa 'kusudi maalum' la kisanaa). Tukizingatia wazo hili tutaona kuwa sehemu ya kwanza ya utenzi huu ina udhaifu wa kutokuwa na maelezo thabiti ya wakati wa zamani. Kwa mfano katika beti za 38—47 mwandishi aelekea kuamini kuwa visiwa vilipojitenga na bara, Mungu alibakiza wanyama wakali bara ili visiwa viwe na amani. Hii haielekei kuwa kweli. Maelezo yanayoelekea kuaminika ni kuwa wanyama wakali waliokuwa visiwani waliuawa wakaisha.

Kuhusu historia msomaji angetegemea watu kama Ibn Batuta na Al- Idrisi kutajwa, vile vile uhusiano wa kiuchumi uliokuwepo kati ya Zanzibar na Ujerumani, Ufaransa, Marekani na Uingereza. Ingawa hatumtegemei mwandishi kutupa historia nzima ya Zanzibar jambo la unyonyaji wa kiuchumi uliofanywa na nchi hizi lisingesahaulika.

Katika beti za 117—119 mwandishi anatueleza kuwa Seyyid Saidi alihamia Zanzibar mwaka 1832. Hii si kweli; Seyyid Said alihamia Zanzibar mwaka 1840. Sababu za kuhamia kwake Zanzibar zimeelezwa vizuri na A.L. Salim katika kitabu chake *The Swahili Speaking Peoples of Kenya's Coast* (uk. wa 15).

Katika sehemu ya tatu mwandishi ameeleza vizuri harakati za ukombozi, lakini jambo ambalo msomaji atajiuliza ni: nani walikuwa viongozi wa kile chama cha mpira, baadaye Chama cha *'African Association'?* Nani walikuwa viongozi wa *Afro-Shirazi?* Viongozi wa Vyama vingine wametajwa. Viongozi ambao wamepewa sifa kubwa baadaye utenzini Abeid Karume na Jumbe - hatuwaoni katika harakati hizi. Wanatokeza ghafla kutoka mahali pasipojulikana.

Katika sehemu ya nne mwandishi ameeleza matukio muhimu katika maendeleo ya nchi, lakini picha anayomwachia msomaji ni kuwa Zanzibar ni sawa na pepo. Ni mahali ambapo udhaifu wa binadamu hauonekani tena na pana uzuri wa kila aina. Mwandishi anatia chumvi katika maelezo yake. Tazama kwa mfano ubeti ufuatao:

Uovu kila namna
Nchini haupo tena
Watu wote wapendana
Imani imeeneya.

Msomaji anaweza kuhisi hapa na pale kuwa mwandishi aliandika utenzi huu kwa madhumuni maalum. Amefikia hata hatua ya kusema:

Chama chetu kwa hakika
Afro iliyotukuka
Kitadumu bila shaka
Mpaka mwisho wa duniya.

'Mwisho wa duniya' haujafika, mwandishi angejiuliza: "tuna Chama gani sasa?" Jibu li wazi kabisa.

Yapo mambo mengine ambayo yanapingana kimantiki. Mwandishi anatwambia katika beti zifuatazo:-

Mengi nimeelezea
Hasa yaliyotokea
Uwongo sikuutia
Hilo nimelikimbiya.

Nimesema ilo kweli
Haki sikuibatili
Nimejipinda kikweli
Uwongo kutoutiya.

Halafu mbele kidogo anasema:-

Kosa likiwa mezuka
Msamaha nautaka
Wasomaji wasifika
Kwenu ninaangukiya.

Jambo la mwisho linahusu nadharia ya maendeleo yaliyofanyika. Katika utenzi mzima mwandishi hakutaja neno "Ujamaa," jambo ambalo linamwacha msomaji akifikiria kuwa maendeleo haya yote yalitokea Zanzibar bila nadharia ya welekeo.

Ingawa utenzi huu una udhaifu kama nilivyoutaja, lakini kazi aliyoifanya mwandishi ni mzuri na itabaki kama kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Huu ni utenzi wa kwanza kuandikwa na mwandishi huyu. Kazi aliyoifanya inatupa tumaini kuwa anao uwezo wa kuandika kazi bora zaidi kama akiendelea na juhudi hii.